

# HALMASHAURI YA WILAYA MUFINDI

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)



S.L.Posts .223

Simu: 026-2772614

FAX: 026-2772070

Email: [dedmufindi@gmail.com](mailto:dedmufindi@gmail.com)

Tarehe 07/03/2017

## TANGAZO LA MNADA WA UUZAJI WA MITI(PAINI) SHAMBA LA MITI –ENEO LA IDARA YA ELIMU MAFINGA

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi anawatangazia Wananchi wote kuwa kutakuwa na mnada wa hadhara wa uuzaji wa miti katika Viunga/Vitalu vya shamba la Halmashauri eneo la Idara la ya Elimu.Mnada huu utafanyika tarehe **27/3/2017 siku ya Jumatatu** kuanzia saa 5:00 asubuhi eneo la Idara ya Elimu Mafinga.

### VIUNGA/VITALU VITAKAVYOUZWA KWA MNADA.

PAINI	
UNENE (CM)	IDADI
≤10cm	
11 - 20	129
21 - 25	94
26 - 30	80
31 - 35	40
≥36	40

2. Kila Kiunga kitanadiwa peke yake kulingana na idadi ya miti iliyopo, Kampuni au mtu Binafsi atakayeshiriki mnada huu atawasilisha nyaraka zake halisi kwa Dalali ikiwa ni pamoja na usajili wa Biashara ya mazao ya misitu na cheti cha utambulisho wa mlipa kodi (TIN). Vielelezo hivi vitakaguliwa kabla ya mnada kuanza.
3. Watu Binafsi na Makampuni wanakaribishwa kutembelea eneo la shamba la miti kwa gharama zao wenyewe siku mbili kabla ya tarehe ya mnada kuanzia saa 3:00 asubuhi hadi saa tisa na nusu (9:30) mchana. Afisa misitu husika atakuwepo shambani kwa ajili ya maelezo zaidi.

**Masharti ya kuzingatia katika mnada huu ni kama ifuatavyo:**

- i) Mnunuzi atakayetaja bei ya juu ndiye atakayepata zabuni husika, pia atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya bei aliyotaja siku ya mnada na itakayobaki italipwa ndani ya siku 14 toka siku ya mnada. Atakayeshindwa kulipia 75% ndani ya siku 14 ile 25% aliyolipa siku ya mnada haitarudishwa.
- ii) Mnunuzi atatakiwa kuvuna miti na kuiondoa katika eneo la shamba ndani ya muda wa siku thelathini (30) kuanzia siku ya kukamilisha malipo ya mwisho yaani 75%.
- iii) Ruhusa ya kuangalia eneo la shamba la miti itatolewa siku mbili (2) kabla ya tarehe ya mnada
- iv) Mnada utaanza saa tano (5:00) asubuhi tarehe 27/03/2017 siku ya **Jumatatu** katika eneo la shamba la miti lililopo Idara ya Elimu Mafinga.

Wote mnakaribishwa,

**Riziki S,Shemdoe (PhD)**  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**MUFINDI**